

JINSI PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY HUFANYA KAZI

Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa katika Washington (WA Notify) ni zana mpya muhimu ya kusaidia kukomesha kusambazwa kwa COVID-19. Kama vile tu kuvaa barakoa, kukaa mbali na watu wengine na kudumisha mikusanyiko ya idadi ndogo ya watu, programu/kipengele cha WA Notify ni zana rahisi ya kulinda jamii yetu.

Programu/kipengele cha WA Notify hufanya kazi kupitia simu mahiri, bila kushiriki maelezo yoyote ya binafsi, ili kuwaarifu watumiaji iwapo huenda wamekaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19. **Ni zana ya faragha kabisa na haikutambui wala kufuatilia utambulisho wako au mahali unapoenda.**

Tafti zimetambua kuwa kadri watu wengi wanavyozidi kutumia arifa za kukaribiana na aliyeambukizwa, ndivyo manufaa yanavyozidi kuwa makubwa. Mifano ya data katika jimbo la Washington inaonyesha kuwa hata kama idadi ndogo ya watu watumia programu/kipengele cha WA Notify, hatua hii itapunguza maambukizi na vifo.

KUWEKA PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY KWENYE SIMU YAKO

Kwenye simu yako ya iPhone:

1. Nenda katika Mipangilio
2. Sogeza chini hadi kwenye sehemu ya Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa
3. Bofya "Washa Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa"
4. Chagua Marekani
5. Chagua Washington


Kwenye simu yako ya Android:

1. Kwenye simu ya Android, nenda kwenye programu ya [Duka la Google Play](#)
2. Tafuta Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa za WA (WA Exposure Notifications) ili upate programu kwa urahisi
3. Pakua programu ya Arifa za Kukaribiana na Aliyeambukizwa katika Washington

BAADA YA KUWEKA PROGRAMU/KIPENGELE CHA WA NOTIFY KWENYE SIMU YAKO


Ifuatavyo ndivyo jinsi programu hufanya kazi ili kusaidia kuzuia kusambazwa kwa COVID-19.

1



Watu wawili wanaotumia programu/kipengele cha WA Notify kwenye simu zao mahiri wanapokuwa wamekaribiana, simu zao hubadilishana misimbo nasibu kwa kutumia Bluetooth. **Msimbo hautambuliki kabisa na haufuatilii mahali mtu alipo au kubadilishana maelezo ya binafsi.**

2



Mtu fulani katika jimbo la Washington anapopatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 na maafisa wa afya wawasiliane naye, ataulizwa iwapo ana programu/kipengele cha WA Notify na kupewa msimbo wa uthibitishaji.

3



Kisha mtu aliyeapatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 ataweka msimbo wa uthibitishaji kwenye programu/kipengele cha WA Notify. Ni hiari ya mtu kufanya hivyo.

4



Mtu yeyote aliye pia na programu/kipengele cha WA Notify na alikaribiana na mtumiaji aliyeapatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 kwa kipindi kirefu cha muda katika siku 14 zilizopita, atapokea arifa isiyomtambulisha mtu yeyote inayomwarifu kuwa huenda ameambukizwa COVID-19.

5



Arifa zina kiungo cha kuelekeza kwa maelezo kuhusu hatua inayofuata unayopaswa kuchukua ili kujilinda na kuwalinda watu wengine. Hazina maelezo yoyote kuhusu mtu aliyeapatikana kuwa ameambukizwa COVID-19 wala mahali ambapo huenda ulikaribiana na mtu aliyeambukizwa COVID-19.